



## MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



### JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

Na: 13. Msimu wa Kilimo 2019/20

Tathmini Februari 1-10, 2019 na Matazamio kwa Kipindi cha Februari 11-20, 2020

#### Muhtasari


- Mvua za nje ya msimu wa *Vuli* zinazoendelea katika maeneo machache yanayopata misimu miwili ya mvua, zinaweza kuathiri uvunaji, ubora na ukaushaji wa mazao.
- Wakulima, wavuvi na wafugaji kwa baadhi ya maeneo wanashauriwa kuchukua tahadhari dhidi ya upepo mkali, unyevunyevu uliokithiri katika udogo na kuwepo kwa wadudu waharibifu katika mazao.

#### MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 1-10, 2020

**K**atika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) iliendelea kudhoofika. Hali hii ilipelekea ukanda wa mvua (ITCZ) kubaki kusini mwa nchi yetu. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani lilionekana kuendelea katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi, hali iliyosababisha kutokea kwa vipindi vifupi vya migandamizo midogo ya hewa. Katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) joto la bahari lilionekana kuwa la juu ya wastani. Hali hii ilipelekea uwepo wa upepo hafifu kuvuma kutoka magharibi hivyo kuwa na mchango mdogo katika kuimarisha mifumo ya unyevunyevu katika anga kutoka katika misitu ya Congo kuelekea katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu.

#### MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 1-10, 2020

**M**ifumo ya hali ya hewa ilichangia uwepo wa mvua katika maeneo mengi ya nchi hususan ukanda unaopata mvua za msimu mara moja mwaka. Kielelezo cha ramani kinaonesha maeneo mengi yanayopata mvua za msimu mara moja kwa mwaka (kusini mwa nchi, nyanda za juu kusini magharibi, na magharibi mwa nchi) yaliweza kurekodi kiwango cha mvua kuanzia 51-150 mm. Hata hivyo, maeneo ya nyanda za juu kaskazini hususan katika mkoa wa Manyara walirekodi mvua kiwango cha chini ya 25 mm. Maeneo machache katika Mikoa ya Ruvuma, Morogoro, Mbeya na Iringa yalirekodi kiwango kikubwa cha mvua zaidi ya 151 mm.



Kielelezo 1: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Februari 1- 10, 2020

#### TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 1-10, 2020

**K**atika dikadi hii, maeneo mengi ya nchi yalikuwa na unyevunyevu wa kutosha. Vipindi vya mvua za nje ya msimu hususan katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua zilichangia ongezeko la unyevunyevu katika udongo hasa katika maeneo ya mabondeni ilisababisha athari katika ukuaji na uvunaji wa mazao.

Maeneo ya Kiteto, Lyamungo, na Morogoro wakulima waliendelea na shughuli ya uvunaji wa mahindi na maharagwe wakati Dodoma, Tanga, Singida, Tabora, na Shinyanga iliripotiwa mahindi yalikuwa

katika hatua ya jani la tisa na wakulima walikuwa wanafanya shughuli ya palizi. Vilevile katika mikoa ya Tanga, Mtwara, Mbeya, na Iringa mahindi yalikuwa katika hatua ya utoaji maua na shunguli za palizi ziliendelea.

Baadhi ya maeneo ya ukanda wa Pwani ya kaskazini (Morogoro, Pemba, na Unguja) wakulima walikuwa katika shughuli za upandaji mpunga. Pia, maeneo ya mkoa wa Simiyu wakulima walijihusisha zaidi na shughuli ya za zao pamba, wakati mkoa wa Mtwara wakulima walijihusisha na usafishaji wa mashamba ya mikorosho. Katika maeneo ya Iringa na Mbeya zao la mahindi lilikuwa katika hatua ya utoaji maua na pia iliripotiwa mkoani Mbeya wakulima walikuwa wanaanda mashamba kwa ajili ya upandaji wa zao la ngano wakati mkoani Njombe walikuwa katika upulizaji wa dawa za kuua panzi na viwavi jeshi.

### HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 1-10, 2020

**K**ina cha maji katika mabwawa, maziwa na mtiririko wa maji katika mito ilikuwa ni nzuri na imara katika ukanda unaopata msimu mmoja wa mvua.

### MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 11-20, 2020.

**M**igandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini inatarajiwa kuendelea kudhoofika. Hali hii inatarajiwa kuendelea kusababisha ukanda wa mvua kubaki kusini mwa nchi. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa kuendelea katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi hali hii inavyotarajiwa kusababisha kutokea kwa vipindi vifupi vya migandamizo midogo ya hewa. Joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii inatarajiwa kupelekea upepo hafifu kuvuma kutoka magharibi hivyo kuwa na mchango mdogo katika kuimarisha mifumo ya nyevunyevu kutoka katika misitu ya Congo kuelekea katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu.

### HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 1-10, 2020.

**K**atika dikadi hii (11-20), baadhi ya maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa), Pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi), na Kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa

Morogoro) yanatarajia kupata mvua zinazoambatana na ngurumo pamoja na vipindi vifupi vya upepo mkali. Kanda ya Ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) yanatarajiwa kupata vipindi vya ngurumo za radi katika maeneo machache.

Maeneo machache ya nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) na pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani, na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) yanatarajia kupata vipindi vya mvua, hususan katika siku tano za mwanzo wa dikadi. Katika upande wa magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) yanatarajia kupata mvua zinazoambatana na ngurumo katika maeneo machache, hususan katika siku tano za mwisho wa dikadi. Pia, baadhi ya maeneo ya kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) yanatarajia kuwepo kwa mvua zinazoambatana na ngurumo.

### HALI YA HEWA KILIMO INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 11-20, 2020.

**M**vua zitarajiwazo katika maeneo mengi ya nchi hususan maeneo yanayopata mvua mara moja kwa mwaka na ukanda wa pwani ya kaskazini zitasaidia ukuaji wa mazao na kuongezeka kwa malisho ya mifugo. Baadhi ya maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua wakulima wanashauriwa kuchukua hatua stahiki ili kulinda mazao yaliyokomaa kutokana na mvua za nje ya msimu wa *Vuli* zinazoendelea. Katika maeneo ambayo yanaunyevu wa juu ya kiwango wakulima wanashauriwa kutumia njia bora za ukaushaji na utunzaji wa mazao.

Wakulima, wavuvi na wafugaji wanashauriwa kufuata ushauri wa maafisa ugani juu ya matumizi sahihi ya madawa na njia uvunaji, ukaushaji na uhifadhi wa mazao. Pia wanashauriwa kuendelea kufuatilia tarifa za Hali ya hewa zinazotolewa na mamlaka (TMA).

### HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 1-10, 2020

**K**ina cha maji katika mabwawa, maziwa na mtiririko ya maji katika mito vinatarajiwa kuimarika. Watumiaji wa maji wanashauriwa kuvuna maji kwa matumizi ya baadae.